SERA G010: SERA YA USAWA WA KIJINSIA NA UWEZESHWAJI WA WANAWAKE

Mtu mwenye wajibu:	CEO	Toleo:	1.1
Imeidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi leo:	27 February 2019	Tarehe ya marekebisho yaliyopangwa:	Februari 2021

UTANGULIZI

Sera hii iliandikwa na Ofisi ya So They Can ya Australia ili itumike katika shughuli zote za So They Can.
So They Can inaendesha taasisi tano ambazo zimesajiliwa nchini Australia, New Zeland, Marekani, Kenya na Tanzania.
So They Can Australia ni ofisi ya kimataifa inayotoa usaidizi kwa taasisi zote za So They Can. Wakati wote Mkurugenzi Mtendaji ina maana ya Mkurugenzi Mtendaji wa So They Can Australia, Kenya na Tanzania. Isipokuwa kama itabainishwa vinginevyo, Bodi ina maana ya Bodi husika ya taasisi ya So They Can ambapo umeajiriwa au ulipopangiwa.

UFAFANUZI

Jinsia ina maana ya tofauti za kijamii kati ya wanawake na wanaume katika mzunguko wa maisha ambaozo watu wanajifunza, na ingawa zimejikita mizizi katika kila tamaduni, zinabadilika baada ya muda, na zinatofautiana kwa kiasi kikubwa ndani ya tamaduni moja na baina ya tamaduni mbalimbali. "Jinsia," pamoja na matabaka na rangi, huamua majukumu, nguvu na rasilimali kwa ajili ya wanawake na wanaume katika utamaduni wowote. Kihistoria, mkazo juu ya mahusiano ya kijinsia imetokana na haja ya kushughulikia mahitaji ya wanawake na hali zao kwa kuwa wao wamekuwa wakinyanyasika zaidi kuliko wanaume. Hata hivyo, kuna ongezeko la jamii kutambua haja ya kujua zaidi kuhusu nini wanaume na wavulana wanakabiliwa wakati wa migogoro.

Usawa wa kijinsia au usawa kati ya wanawake na wanaume, inamaanisha wanawake, wasichana, wavulana na wanaume kufurahia kwa usawa haki zao, fursa, rasilimali na tuzo. Usawa wa kijinsia haumaanishi kwamba wanawake na wanaume hawana tofauti, lakini kufurahia haki zao, fursa na nafasi za kimaisha haziongozwi au kutatizwa kuzaliwa kwao wanawake au wanaume.

Haki za kijinsia inamaanisha haki katika mgawanyo wa rasilimali, faida/matunda na majukumu kati ya wanawake na wanaume, wavulana na wasichana. Dhana hii inatambua kwamba hakuna usawa katika mahusiano ya kimamlaka kati ya wasichana na wavulana, wanaume na wanawake, na kwamba suala kutokuwa na usawa linapaswa kushughulikiwa.

Vurugu zinazotokana na jinsia ni dhana mwavuli(ya ujumla) inayoashiria tendo lolote lenye madhara analofanyiwa mtu kinyme na mapenzi yake kutokana na tofauti zilizowekwa na jamii kati ya mwanamke na mwanaume. Hali na kiwango cha aina maalum za vurugu zinazotokana na jinsia hutofautiana kati ya

tamaduni mbalimbali, nchi na maeneo. Mifano ni pamoja na unyanyasaji wa kijinsia, ikiwa ni pamoja na unyonyaji / unyanyasaji wa ngono na ukahaba wa kulazimishwa; unyanyasaji majumbani; biashara haramu ya binadamu; ndoa za kulazimishwa / za mapema; tamaduni mbaya kama vile ukeketaji wa wanawake; mauaji; na urithi wa mjane.

Uwezeshwaji wa wanawake unahusisha kukuza ufahamu, kujenga uwezo wa kujiamini, upanuzi wa uchaguzi, kuongeza upatikanaji na uthibiti wa rasilimali na vitendo vya kubadilisha miundo na taasisi zinazoimarisha na kuendeleza ubaguzi na utofauti wa kijinsia. Uwezeshwaji unatoka ndani; wanawake wanajiwezesha wenyewe. Ongeza nguvu za wanawake kwa nguvu ya; nguvu pamoja na nguvu kutoka ndani ambayo inazingatia kutumia watu binafsi na uwezo wa pamoja kufanya kazi kwa malengo ya kawaida bila kulazimishwa. Uwezeshwaji wa wanawake unafanikiwa wakati wanawake na wasichana wanapata uwezo wa kutumia haki zao, kutenda kwa uhuru na kutimiza uwezo wao kama wanajamii kamili na sawa wa jamii yao.

SERA

Sera Usawa wa Jinsia na Uwezeshwaji wa Wanawake inalingana na Lengo la Tano la Umoja wa Mataifa la Maendeleo - Kufikia usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake na wasichana wote - na inaendana na mkakati wa uwiano wa kijinsia na mkakati wa uwezeshaji wa wanawake wa Serikali ya Australia
Madhumuni ya Sera hii ni kutoa maelekezo kwa So They Can na washirika wake kupanga kimkakati na kufanikisha malengo ya usawa wa kijinsia ndani ya mipango, taratibu na mifumo ya mashirika, majukumu na uwajibikaji.
Usawa wa jinsia na Uwezeshaji wa Wanawake iwe msingi katika kubuni, utekelezaji, uendeshaji na tathmini ya miradi na shughuli zote za So They Can katika nchi zote ambako So They Can inafanya kazi.

KANUNI

So They Can inatambua jukumu muhimu la wanawake wanalofanya katika kuharakisha maendeleo na kwa kupitisha sera hii inakusudia kutekeleza misingi ya usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake ulioandaliwa na Wanawake wa Umoja wa Mataifa:

- Kuanzisha uongozi wa juu wa usawa wa kijinsia wa taasisi.
- kuwatendea wanawake na wanaume kwa haki kazini-kuheshimu na kusapoti haki za binadamu na kutokuwepo kwa ubaguzi.
- Kuhakikisha afya, usalama na ustawi wa wafanyakazi wote wanawake na waume.
- Kukuza elimu, mafunzo na maendeleo ya kitaalamu kwa wanawake.
- Utekelezaji wa maendeleo ya taasisi, ugavi na taratibu za masoko ambazo huwezesha wanawake.
- Kukuza usawa kupitia mipango ya jamii na utetezi.
- Kupima na kuripoti hadharani juu ya maendeleo ili kufikia usawa wa kijinsia.

TARATIBU

Kwa kuzingatia usawa wa jinsia na Uwezeshaji wa Wanawake, So They Can inakusudia:

- kupitisha mbinu zenye mlengo wa haki za kushughulikia masuala ya kijinsia ambayo inalenga na kutetea haki za wanawake na wasichana na kuandaa mifano bora katika haki ya kijinsia;
- kuongeza uwezo wa wanawake na wasichana wa kutambua haki zao, kuamua mwelekeo wa maisha yao na kushawishi maamuzi katika kaya, jamii na jamii zao;
- kuondoa utofauti wa usawa wa kijinsia katika upatikanaji, kudhibiti na kufaidika na rasilimali, elimu na huduma za afya na fursa za ajira;
- kuhakikisha ushiriki sawa wa wanawake katika mashauriano ya jamii, mchakato wa kufanya maamuzi katika kubuni na utekelezaji wa mipango;
- kuhakikisha kwamba usawa wa kijinsia unazingatiwa katika kila hatua ya mzunguko wa mradi ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji na tathmini;
- uchambuzi wa changamoto za kiusalama na utekelezaji wa mikakati ya kuzishughulikia kuzuia madhara kwa wanawake, wasichana, wavulana na wanaume.
- kuhamasisha usawa wa jinsia katika vikundi vyote vya kazi na mipango;
- Kuondoa aina zote za ubaguzi wa kijinsia, umri na mambo mengine tofauti kama vile ukabila, dini, nk.
- kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia na kupunguza madhara yake kwa watu binafsi na jamii;
- kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake kupitia miradi na mipango maalum;
- kusaidia wanawake katika kufikia nafasi za uongozi katika jamii zao;
- kuhakikisha kuwa mafunzo ya usawa wa kijinsia na ya uwezeshaji wa wanawake hutolewa kwa wafanyakazi wote wa mradi;
- kufanya kazi na washirika ili kuendeleza vipaumbele vya usawa wao wa kijinsia

RELATED DOCUMENTS

- So They Can Policy and Manual Register
- DFAT Gender Equality and Women's Empowerment Strategy (February 2016)
- ACFID Code of Conduct, Commitment 2.3 We promote Gender Equality and Equity